# UTAFITI WA MATUMIZI YA LUGHA

Mpendwa Mzazi/Mlezi:

Kuzungumza zaidi ya lugha moja ni rasilimali muhimu. Tunazihimiza familia kudumisha lugha yao (zao) ya asili huku wanapojifunza Kiingereza. Wanafunzi wanaozungumza au kuelewa lugha nyingine huenda wakastahiki usaidizi wa kuboresha Kiingereza chao na kusaidia kutimiza viwango vya kielimu vya Maine. Maswali yafuatayo, yanayohitajika kwa wanafunzi wote kutoka shule ya watoto wachanga hadi darasa la 12, yatasaidia shule yako kuamua ikiwa mtoto wako atafaidika kutokana na huduma za usaidizi za lugha ya Kiingereza.

Ikiwa ungependa barua hii na utafiti ulio hapa utolewe katika lugha nyingine, au ikiwa ungependa mkalimani, shule yako itatimiza maombi hayo. Una haki ya kisheria ya kupata mawasiliano yoyote kutoka shuleni kwa njia ya maneno ya kinywa au kwa kuandika katika lugha unayoweza kuielewa vyema.

Ikiwa lugha nyingine kando na Kiswahili imeonyeshwa hapa chini, mtoto wako atakamilisha uchunguzi wa ufasaha wa lugha ya Kiingereza (ELP). Kulingana na mafanikio ya mtoto wako, huenda mtoto wako akatambuliwa kama Mwanafunzi wa Kiingereza na anayestahiki usaidizi wa lugha ya Kiingereza. Kuwa na uhakika kwamba, majibu yako yatatumika tu kwa madhumuni ya kielimu na kuwekwa kwenye faili ya shule ya mtoto wako, inayofikiwa na wafanyakazi wa shule pekee. Wafanyakazi wa shule hawaruhusiwi kuuliza kuhusu hali ya uhamiaji ya familia yako.

Asante kwa kutoa maelezo haya na kila la heri kwa ufanisi wa kielimu wa mtoto wako.

| | |
|---|---|
| Jina la Mwanafunzi: | Tarehe ya Kuzaliwa: |
| Shule: | Darasa Linalotarajiwa: |

**Tafadhali usikose kujibu swali lolote.**

1. Je, ni lugha ipi (zipi) ambayo mtoto wako alizungumza au kuelewa mara ya kwanza? ______________________

2. Je, ni lugha ipi (zipi) ambayo mtoto wako huzungumza au kuelewa kwa urahisi? ______________________

3. Je, ni lugha ipi (zipi) ambayo watu hutumia wanapozungumza na mtoto wako kila siku? ______________________

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ______________________________ Tarehe: ______________

---

**Utambulisho wa Baada ya Kujisajili kwa Matumizi ya Shule Pekee**: <u>Ikiwa Kiingereza ndiyo lugha ya pekee iliyotambulishwa kwenye Utafiti wa Matumizi ya Lugha (Maswali 1-3 yaliyo hapo juu)</u>, uchunguzi wa ELP huenda ukaendelezwa **<u>tu iwapo</u>** sehemu hii imejazwa na mwalimu na kisha kuidhinishwa na Mkurugenzi/Mratibu wa Lugha Nyingi au Kamati ya Ufikiaji wa Lugha. Fafanua ushahidi kuwa maendeleo ya lugha ya Kiingereza ya mwanafunzi yameathriwa na lugha yake ya msingi au ya nyumbani kando na Kiingereza.

**Saini:** Mwalimu ______________________________ Tarehe: ______________

Mkurugenzi/Mratibu wa Lugha Nyingi ______________________________ Tarehe: ______________

WEKA NAKALA HALISI YA HATI HII ILIYOJAZWA KWENYE FOLDA YA KUDUMU YA REKODI YA MWANAFUNZI

Msingi wa Kisheria: Sehemu ya 3111, Sheria ya 1965 ya Elimu ya Shule ya Msingi na Ya Shule ya Upili